NISHATI | HABARI ZA NISHATI
News Bulletin
www.nishati. go.tz Wizara ya Nishati wizara_ya_nishati_tanzania @Nishati2017 Wizara ya Nishati
Toleo Namba 12 Machi 1-31, **2020**

# TANZANIA INAONGOZA AFRIKA UUNGANISHAJI UMEME VIJIJINI – DKT KALEMANI



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa kijiji cha Nagaga, Kata ya Namalenga, wilayani Masasi, Mkoa wa Mtwara wakati wa hafla ya kuwasha rasmi umeme kijijini hapo, Februari 13, 2020.*

UK. 2

# WATAALAMU SADC WAJADILI UPATIKANAJI NISHATI TOSHELEVU KWA NCHI WANACHAMA

JARIDA HILI LINATOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI
Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma

# TANZANIA INAONGOZA AFRIKA UUNGANISHAJI UMEME VIJIJINI – DKT KALEMANI

*Veronica Simba – Masasi*

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, amebainisha kuwa kwa sasa, Tanzania inashika nafasi ya kwanza katika kuunganisha umeme vijijini ikiwa imefikia asilimia 74 ya vijiji vyote.

Ameyasema hayo Februari 13 mwaka huu, wakati akizungumza na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, akiwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme.

"Awali, Nigeria ndiyo ilikuwa ikiongoza ikiwa na asilimia 72 lakini tumeipita, tukiwa tumefikia zaidi ya asilimia 74 na hivyo tunaongoza Afrika kwa sasa," amesema Waziri.

Akieleza zaidi, Dkt Kalemani amesema kuwa, jumla ya vijiji 9,001 nchini vimeshaunganishiwa umeme na kwamba, kati ya hivyo, vijiji 3,559 vimeunganishiwa umeme kupitia Mzunguko wa kwanza wa Awamu ya Tatu ya Mradi wa Umeme Vijijini (REA III-1), unaoendelea hivi sasa.

Amesema, Mradi wa REA III-1 utakamilika Juni mwaka huu lakini serikali imekubaliana na wakandarasi wote wanaotekeleza mradi huo nchi nzima, kukamilisha kazi husika miezi miwili kabla, hivyo wanatarajiwa kukabidhi kazi kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), ifikapo Aprili 31, 2020.

Kwa upande wa Wilaya ya Masasi pekee, Dkt Kalemani ameeleza kuwa serikali iliamua kurejea mpango-kazi na kufanya mabadiliko ambayo yaliwezesha kuongeza idadi ya vijiji vitakavyonufaika na mradi huo wilayani humo.

"Niwe mkweli kuwa, katika mpango wa awali, ni vijiji vichache tu vya Masasi ndivyo vilikuwa vinufaike na mradi huu. Hii ni kwa sababu vijiji vingine viko katika Halmashauri za Miji na siyo Wilaya hivyo vilikuwa vinakosa sifa kwani vilikuwa na hadhi ya Mitaa na siyo vijiji."



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akimpongeza mmoja wa wakazi wa kijiji cha Matogolo, Kata ya Mbuyuni, wilayani Masasi, Mkoa wa Mtwara, baada ya kumuwashia umeme kwenye nyumba yake, Februari 13, 2020.*

Aliendelea kubainisha kuwa, kwa ushawishi na jitihada za Mbunge wa eneo hilo, Rashid Chuwachuwa, serikali iliamua kufanya marejeo na kuongeza idadi ya vijiji katika mpango wa REA, husussan vile vilivyo na taswira ya miji-vijiji, yaani ni mitaa lakini kiuhalisia maisha ya watu wake ni sawa na walioko vijijini.

Akijibu hoja za wananchi wa vijiji vya Namikunda A na B, Nagaga na Matogolo kuhusu changamoto ya umeme kukatika mara kwa mara, Waziri, kwa nyakati tofauti alieleza kuwa tayari serikali imeshughulikia tatizo hilo kwa kuunganisha baadhi ya maeneo ya Mtwara katika gridi ya Taifa.

Ameyataja maeneo hayo kuwa ni Tunduru, Masasi na Nanyumbu na kwamba yameunganishwa kupitia mradi wa umeme mkubwa wa Makambako – Songea (kilovoti 220).

Katika ziara hiyo ambayo Waziri aliviwashia umeme vijiji vya Nagaga na Matogolo, ametoa hamasa kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kulipia ili waunganishiwe umeme.

Aidha, ametoa onyo kali kwa mameneja wa TANESCO nchi nzima ambao wanalalamikiwa kutopokea malipo ya wananchi wanaohitaji huduma ya umeme kwa madai kuwa hakuna vifaa au sababu nyingine ya aina hiyo, huku akiweka wazi kuwa watakaobainika, watachukuliwa hatua kali.

Waziri amewataka wananchi kutumia simu zao za mkononi kuwapiga picha na kuwarekodi mameneja wanaogoma kupokea malipo husika wakati umeme umeshafika kwenye maeneo yao na kuziwasilisha wizarani kama ushahidi ili wachukuliwe hatua za kinidhamu.

"Kamwe hatutawavumilia mameneja wa aina hiyo kwa sababu siyo tu wanalikosesha shirika mapato lakini pia wanaichonganisha serikali na wananchi kwa kuchelewa kuwapatia huduma husika," amesisitiza.

Katika hatua nyingine, Dkt Kalemani amewasihi wananchi kuwa wavumilivu pale inapotokea huduma ya umeme imekatwa hususan katika kipindi hiki cha mvua huku akieleza kuwa hali hiyo inasababishwa na kufanya ukarabati wa miundombinu ambayo imekuwa ikiathiriwa na mvua.

Hata hivyo, amewataka watendaji wa TANESCO kuhakikisha wanatoa taarifa kwa wananchi kwa wakati pindi wanapolazimika kukata umeme ikiwa ni pamoja na kufanya matengenezo hayo kwa muda mfupi ili kurejesha huduma ya umeme kwa wananchi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee pamoja na Mbunge, Rashid Chuwachuwa, wamepongeza uwajibikaji wa serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli, ambao umekuwa na matokeo chanya kwa wananchi.

Katika ziara hiyo, Waziri aliambatana na viongozi na wataalamu mbalimbali wa Wizara, TANESCO na REA.





# BODI YA UHARIRI

**Mhariri**
**Veronica Simba**
(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini)

**Waandishi**
**Veronica Simba**
**Teresia Mhagama**
**Zuena Msuya**
**Hafsa Omar**

**Msanifu Kurasa**
**Lucas Gordon**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148 au

Fika Ofisi ya Mawasiliano Mtumba Dodoma, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma

*www.nishati. go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*


## KWAHERI DKT MWINYIMVUA, KARIBU MHANDISI ZENA NA MHANDISI MASANJA

Februari 3 mwaka huu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Pombe Magufuli, aliwaapisha viongozi wa Serikali aliowateua kushika nyadhifa mbalimbali.

Miongoni mwa walioapishwa ni Mhandisi Zena Said ambaye ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati pamoja na Mhandisi Leonard Masanja, aliyeteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara yetu.

Mhandisi Zena amechukua nafasi ya Dkt Hamisi Mwinyimvua, ambaye amestaafu utumishi wa umma kwa mujibu wa sheria.

Katika mapokezi maalumu ya viongozi hao wizarani, yaliyofanyika Februari 7 mwaka huu, wafanyakazi wote wa Wizara wakiongozwa na Waziri Dkt Medard Kalemani na Naibu Waziri Subira Mgalu, walionesha imani kubwa kwa viongozi hao wapya na kuahidi kuwapatia ushirikiano katika kutekeleza majukumu yao.

Sisi wa Nishati News Bulletin, tunawiwa kuwasihi wasomaji wa Jarida hili na wadau wetu wote wa sekta ya nishati, kuungana na viongozi na wafanyakazi wa Wizara na Taasisi zake, katika kuwapatia ushirikiano viongozi wetu wapya, kila mmoja kwa nafasi yake, ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kulitumikia Taifa letu ipasavyo.

Tukumbuke usemi usemao 'Umoja ni nguvu, Utengano ni udhaifu' hivyo basi Umoja wetu ndiyo nguvu yetu. Pamoja na kwamba viongozi wetu hawa, wana sifa nyingi za kiutendaji na kitaaluma, pasipo kuwapa ushirikiano, itawawia vigumu kuyatekeleza yale waliyotumwa na Mheshimiwa Rais ambayo kwa ufupi yanalenga kuhakikisha Watanzania wananufaika kupitia sekta ya nishati.

Kwa upande mwingine, kwa niaba yenu nyote wana-familia ya Nishati, tunawiwa kumpongeza na kumshukuru Katibu Mkuu Mstaafu, Dkt Hamisi Mwinyimvua, ambaye ametimiza wajibu wake ipasavyo wakati wa utumishi wake, ambao sote tunajivunia.

Tunafarijika kwakuwa Katibu Mkuu mpya pamoja na Naibu wake, wameahidi kuendeleza jitihada zake pale alipoishia na katika hilo tunayo imani kubwa kuwa wataiishi ahadi hiyo kwani historia yao ya utendaji kazi inadhihirisha uwezo wa kila mmoja wao.

Tunahitimisha kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani aliyoionesha kwa viongozi wetu hawa na kuwateua kushika nyadhifa hizo.

Kwaheri Dkt Mwinyimvua. Karibu katika familia ya Nishati Mhandisi Zena na kwako Mhandisi Masanja tunasema pongezi kwa wadhifa mpya (maana wewe umekuwa katika familia hii tangu kitambo ukitumikia nafasi mbalimbali). Sisi Nishati tunaamini katika uchapaji kazi na ndiyo maana hujipambanua kwa kusema Nishati Tuko Kazini. Haya shime, tuchape kazi.

# Katunika Ki-nishati



# MATUKIO PICHANI







*Said Maleka na mkewe Zainab Seleman, wakazi wa kijiji cha Nagaga, Kata ya Namalenga, wilayani Masasi, Mkoa wa Mtwara, wakiwa na kifaa cha Umeme Tayari (UMETA), nje ya nyumba yao baada ya kupewa kifaa hicho na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) ili kitumike kuwaunganishia umeme ikiwa ni ishara ya dhamira ya dhati ya serikali kutobagua nyumba wakati wa kuunganisha nishati hiyo. Waziri aliwasha rasmi umeme kijijini hapo Februari 13, 2020.*

*Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, akiwasilisha kwa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, taarifa ya hali ya upatikanaji umeme wilayani humo. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi kukagua utekelezaji wa miradi ya umeme Februari 13, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akiwatambulisha kwa wananchi, viongozi na wataalamu mbalimbali kutoka wizarani, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), wakati wa hafla ya uwashaji rasmi umeme katika kijiji cha Nagaga, wilayani Masasi, Mkoa wa Mtwara, Februari 13, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia), akiwakabidhi kifaa cha Umeme Tayari (UMETA), Zainab Selemani (kushoto) na mumewe Said Maleka, wakazi wa kijiji cha Nagaga, wilayani Masasi, Mkoa wa Mtwara ili kitumike kuwaunganishia umeme katika nyumba yao ya nyasi (haipo pichani) ikiwa ni kudhihirisha dhamira ya serikali ya kuwaunganishia umeme wananchi wote pasipo kujali aina ya makazi yao. Waziri aliwasha rasmi umeme kijijini hapo Februari 13, 2020.*

# WATAALAMU SADC WAJADILI UPATIKANAJI NISHATI TOSHELEVU KWA NCHI WANACHAMA

*Zuena Msuya - Dar es salaam*

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, amesema Mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati kwa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) unalenga kuanzisha mtandao wa upatikanaji umeme wa uhakika, wa kutosha na gharama nafuu ili kuchochea ukuaji wa uchumi na viwanda katika jumuiya hiyo.

Mhandisi Said alisema hayo baada ya kufungua mkutano wa siku nne uliofanyika Februari 25 hadi 28, 2020, jijini Dar es Salaam na kuwakutanisha Watalaamu na Makamishina wa Nishati kutoka nchi 12 wanachama wa SADC ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa uamuzi uliopitishwa na Wakuu wa Nchi husika pamoja na Mawaziri wake wanaosimamia masuala ya nishati.

Alisema kwa mujibu wa taarifa zilizopo, mahitaji ya umeme kwa nchi za ukanda huo yanatarajiwa kuongezeka kutoka kiwango cha Terawatt 300 hadi Terawatt 580 kwa saa ifikapo mwaka 2030.

Aidha, alisema kuwa, vyanzo vya nishati vilivyopo kwa sasa katika nchi za SADC, vinaweza kuzalisha nishati kwa kutumia jotoardhi (megawati 15,000), upepo (megawati 110,000), maji (megawati 350,000) na jua (megawati milioni 10).



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, akizungumza wakati akifungua Mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati kwa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) uliofanyika jijini Dar es Salaam Februari 25 hadi 28, 2020*

Aliongeza kuwa, pamoja na utajiri wa vyanzo vya nishati barani Afrika, nchi nyingi za Jumuiya hiyo bado zinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa nishati ya kutosha.

Vielevile, alibainisha kwamba, katika mkutano huo, wataalamu hao walijadili na kuafikiana kuwa nchi zitakazozalisha nishati kwa wingi na endelevu, inayokidhi mahitaji ya matumizi ya ndani na ziada, iwauzie wengine kama biashara nyingine zinavyofanyika

Pia, alisema kumegundulika kiwango kikubwa cha gesi katika nchi kadhaa ikiwemo Tanzania na Msumbiji.

"Mahitaji ya mafuta na gesi pia yataongezeka, katika sekta zote ikiwamo viwanda, usafiri, taasisi na makazi katika ukanda huo. Sasa tunaelekea kuzalisha umeme mwingi na gharama nafuu ambao utasaidia kupunguza matumizi ya nishati ya mkaa na hatimaye mabadiliko ya tabia yanayotuletea majanga mbalimbali kama vile mafuriko yataondoka," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa mkutano huo ambaye pia ni Kamishna wa Petroli na Gesi (Tanzania), Adam Zuberi alisema kuwa, hoja zilizojadiliwa ni pamoja na uanzishaji wa Kituo cha Umahiri cha kuendeleza nishati jadidifu, matumizi bora ya nishati kwa nchi za jumuia hiyo, mapitio ya itifaki ya nishati ya 1996 pamoja na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa utekelezaji wa matumizi bora ya gesi asilia katika nchi za SADC.

Pia, alisema mkutano ulifanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Sekta ya Nishati chini ya Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Miundombinu katika Mtangamano (RIDMP), utakaokoma 2027.

Zuberi alisema kuwa baada ya kukamilika kwa mkutano huo, kamati husika itaandaa ripoti itakayowasilishwa na baadaye kujadiliwa katika Baraza la Mawaziri wa masuala ya nishati itakapofika mwezi Mei, mwaka huu.

Mkutano wa 39 wa jumuiya hiyo ulifanyika Agosti 17 na 18, 2019, jijini Dar es Salaam na kukabidhi majukumu ya uongozi wa jumuiya hiyo kwa Rais wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli baada ya Rais wa Namibia, Hage Geingob kumaliza muda wake.

Baada ya tukio hilo, Tanzania ilianza kuratibu na kusimamia vikao mbalimbali vya kamati za watalaamu kutoka sekta mbalimbali vitakavyoendelea katika ngazi ya mawaziri.



*Kamishna wa Petroli na Gesi kutoka Wizara ya Nishati (Tanzania), Adam Zuberi akizungumza na washiriki wa Mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati kwa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) uliofanyika jijini Dar es Salaam Februari 25 hadi 28, 2020.*




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (katikati waliokaa), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati kwa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) uliofanyika Jijini Dar es Salaam, Februari 25 hadi 28, 2020.*

# MATUKIO PICHANI





*Washiriki wa Mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati kwa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) uliofanyika jijini Dar es Salaam, Februari 25 hadi 28, 2020 wakimsikiliza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (hayupo pichani) wakati akifungua mkutano huo.*




*Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Mbadala, Edward Ishengoma (katikati) na Kamishna Msaidizi wa Umeme Mhandisi Innocent Luoga (wa pili - kushoto), wakifuatilia majadiliano katika mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati kwa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) uliofanyika jijini Dar es Salaam, Februari 25 hadi 28, 2020.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati kwa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC), Mhandisi Styden Rwebangila (kushoto) na Mwenyekiti wa kamati ndogo ya maudhui ya mkutano huo, Emilian Nyanda (katikati) wakibadilishana mawazo na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Umahiri cha uendelezaji wa nishati jadidifu na matumizi bora ya nishati kutoka nchini Namibia, Kudakwashe Ndhlukula.*

*Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka (wa tatu - kulia), akifuatilia mada katika Mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati kwa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) uliofanyika jijini Dar es Salaam, Februari 25 hadi 28, 2020.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (wa pili - kulia), Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuber (kushoto) na Mkurugenzi wa Masuala ya Miundombinu wa SADC (wa pili - kushoto), wakifuatilia majadiliano katika mkutano Wataalamu wa Masuala ya Nishati kwa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika, uliofanyika jijini Dar es Salaam kuanzia Februari 25 hadi 28, 2020.*



*Kamishna Msaidizi wa Maendeleo ya Umeme, Mhandisi Styden Rwebangila (katikati) akifuatilia majadiliano katika Mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati kwa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) uliofanyika jijini Dar es Salaam, Februari 25 hadi 28, 2020.*




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, (kulia) na Mkurugenzi wa masuala ya Miundombinu wa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC), Mapalao Makoena, wakijadiliana wakati wa Mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati wa SADC, uliofanyika jijini Dar es Salaam Februari 25 hadi 28, 2020.*



# MGALU AITAKA EWURA KUHARAKISHA UANDAAJI KANUNI KWA WAWEKEZAJI BINAFSI WA UMEME

**Hafsa Omar - Pwani**

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, ameitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kuharakisha uandaaji wa kanuni ambazo zitatumika kudhibiti bei za umeme kwa ajili ya wawekezaji binafsi wa umeme nchini.

Aliyasema hayo, Februari 20, 2020 wakati alipokuwa akijibu maswali mbalimbali ya wananchi kuhusu gharama kubwa ya umeme wanayotozwa na Mkandarasi wa kampuni ya Husk Power iliyopo katika kijiji cha Matipwili, kata ya Mkange, Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani.

Alisema, EWURA inatakiwa kuyafanyia kazi maelekezo hayo kwa haraka ili wawekezaji hao wadogo, wapate mwongozo husika utakaowasaidia kufanya kazi kwa kufuata sheria za nchi pasipo kujichukulia maamuzi ya kujiwekea bei za juu ambazo zinawaumiza Watanzania wa kipato cha chini.

Alifafanua kuwa, serikali ilitoa fursa kwa wawekezaji hao kuwapelekea umeme Watanzania ambao wapo katika maeneo yaliyo mbali na gridi ya Taifa na kwamba, iliamua kutoa ruzuku ili wawekezaji hao watoe bei nafuu ya umeme kwa wananchi wa kipato cha chini.

"Ni kweli wao wamewekeza miundombinu yao hapo, lakini haiwezekani wananchi walipishwe shilingi 5,000 kwa siku. Pia, haiwezekani shilingi 350,000 iwe bei ya mtumiaji wa kioski. Hilo hapana. Gharama hiyo ni sawa na ya umeme unaotumika kwenye kiwanda cha ukubwa wa kati," alisema Mgalu.

Alieleza kuwa, Serikali ina jukumu la kuwalinda watumiaji wa nishati nchini na kwamba, kwa kuzingatia jukumu hilo, inawakumbusha wawekezaji kuwa bei ya kuunganisha umeme vijijini ni shilingi 27,000 tu.

"Tunataka wapunguze gharama za uendeshaji, watumie wataalamu wa ndani, watumie vifaa vya ndani ili gharama za uendeshaji zishuke na watanzania wapate unafuu, vinginevyo gharama za umeme zisiposhuka sisi tutakwenda hata maeneo ambayo tulisema waende wao na watakosa fursa hii. Hatutakubali bei kama hizo," alisema

Aidha, alimtaka mkandarasi huyo kukutana na Meneja wa TANESCO Mkoa wa Pwani ili kujadiliana na kuzipitia tena bei za umeme ambazo anazitumia kwa lengo la kupata uwiano wa bei za umeme kwa manufaa ya Watanzania wote.



*Mkazi wa kijiji cha Matipwila. Kata ya Mkange, Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani akitoa maoni kuhusu umeme kwa Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (hayupo pichani), wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini humo hivi karibuni.*



*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Matipwila, Kata ya Mkange, Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, alipokuwa katika ziara ya kazi kukagua usambazaji umeme.*

*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (wa pili kushoto), akisikiliza maoni na kero za wananchi wa kijiji cha Matipwili, Kata ya Mkange, wilayani Bagamoyo, kuhusu umeme. Alikuwa katika ziara ya kukagua usambazaji umeme hivi karibuni.*



# SERIKALI YADHAMIRIA KUPELEKA UMEME WA GRIDI KAGERA YOTE





*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (aliyeinua mkono), akitoa maelekezo mbalimbali kwa uongozi wa TANESCO, yanayohusu kuboresha huduma ya upatikanaji umeme kwa wananchi, alipotembelea Kituo cha kupoza umeme Kyaka, kilichopo wilayani Misenyi, Mkoa wa Kagera, Februari 27 mwaka huu. Wa kwanza kulia ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Luteni Kanali Dennis Mwila.*

***Veronica Simba – Kagera***

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amesema Serikali imedhamiria kupeleka umeme wa gridi ya Taifa katika Mkoa wote wa Kagera, awamu kwa awamu ikianza na Wilaya za Bukoba Vijijini, Muleba na Misenyi.

Amesema Wilaya hizo za awali zitaungwa kwenye gridi ya Taifa ndani ya kipindi cha mwezi mmoja kutoka sasa.

Waziri ameeleza hayo Februari 27 mwaka huu wakati akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Generali Marco Gaguti, akiwa katika ziara ya kazi.

"Wataalamu wetu kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wataanza kujenga njia ya kusafirisha umeme wa kilovoti 33 kutoka Kanazi mpaka Itako na kutoka Itako mpaka Misenyi," amefafanua.

Akieleza zaidi, amesema maeneo hayo yataanza kutumia umeme wa gridi ya Taifa inayotoka Geita mpaka maeneo ya Ngara, Biharamulo na baadaye Misenyi.

Hata hivyo, Waziri amesema maeneo ambayo hayatafikiwa katika awamu ya kwanza kikiwemo kiwanda cha sukari cha Kagera na mengine yote yatakayosalia, yataendelea kutumia umeme kutoka nchi jirani ya Uganda wakati wakisubiri awamu nyingine ya utekelezaji wa mpango huo.

Akielezea kuhusu kuyaunga maeneo hayo yatakayosalia, Waziri amesema zoezi hilo litafanyika baada tu ya kukamilika kwa miradi mikubwa ya umeme ya Kakono, Rusumo na Nyakanazi.

"Miradi hiyo ikikamilika, taratibu tutaweza kuwaondoa wale waliosalia kutoka kwenye gridi ya Taifa upande wa Uganda na kuwaunga kwenye gridi ya Taifa ya hapa nchini."

Aidha, Waziri amebainisha kuwa, utekelezaji wa mpango huo ni sehemu ya mkakati wa serikali unaoendelea ukilenga kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo yote ya nchi yetu.

Ameeleza zaidi kuwa, mbali ya kuimarisha hali ya upatikanji umeme nchini, serikali pia inapanga kuwa na umeme mwingi utakaotosheleza mahitaji ya ndani na kuuza ziada kwa nchi jirani za Ukanda wa Afrika Mashariki.

"Leo sisi tunanunua umeme kutoka kwa jirani zetu. Tunataka nasi tuwauzie umeme hapo baadaye. Uhakika wa kufanya hivyo tunao kutokana na miradi mikubwa tunayoitekeleza ukiwemo ule wa kuzalisha umeme (megawati 2,115) wa Julius Nyerere huko Rufiji."

Kwa upande wake, Brigedia Gaguti amepongeza uamuzi huo wa serikali kuunganisha umeme wa gridi ya Taifa katika Mkoa wote wa Kagera na kuahidi kutoa ushirikiano kadri utakavyohitajika katika kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kikamilifu.

Katika ziara hiyo ya siku moja, Waziri na Ujumbe wake walitembelea maeneo mbalimbali ambayo yatahusika katika utekelezaji wa Mradi huo kikiwemo kituo cha kupoza umeme cha Kyaka kilichopo wilayani Misenyi.



*Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Generali Marco Gaguti (kushoto), akimweleza jambo Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia). Waziri na Ujumbe wake walifika ofisini kwa Mkuu wa Mkoa kumweleza dhamira ya ziara yake mkoani humo, Februari 27 mwaka huu.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake, wakikagua kituo cha kupoza umeme Kyaka, kilichopo wilayani Misenyi, Mkoa wa Kagera, alipokuwa katika ziara ya kazi Februari 27 mwaka huu.*

# NAIBU WAZIRI ARIDHISHWA NA KASI YA USAMBAZAJI UMEME KATIKA TAASISI ZA UMMA

***Hafsa Omar - Lindi***

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amefurahishwa na kuridhishwa na kasi ya uunganishwaji umeme kwenye Taasisi za Umma zilizopo wilayani Liwale, Mkoa wa Lindi, kama serikali ilivyoagiza.

Alisema hayo kwa nyakati tofauti, Februari 24 mwaka huu, wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Liwale mjini na wa kijiji cha Makata, Kata ya Makata, Wilaya ya Liwale, kabla ya kuwasha umeme katika Zahanati ya Kijiji pamoja na Shule ya Msingi Nalueho.

Aidha, alisema ziara yake mkoani humo ililenga kukagua kazi za usambazaji umeme zinavyoendelea katika Mkoa huo pamoja na kujionea mwenyewe kasi ya usambazwaji wa umeme katika taasisi za umma kufuatia agizo la serikali kutaka zipelekewe umeme.

Naibu Waziri alikiri kufurahishwa kuona shule na zahanati nyingi za Wilaya hiyo zikiwa zimeunganishiwa huduma hiyo.

"Rais Dkt. John Pombe Magufuli aliagiza tunapopeleka umeme vijijini, tuunganishe kwenye taasisi za umma hususani shule, zahanati, vituo vya afya, miradi ya maji, ofisi za serikali na kadhalika, hivyo nimefurahi leo tunawasha umeme kwenye shule ya msingi ambayo watoto wetu wanasoma," alisema.

Alisema, lengo la kupeleka umeme kwenye taasisi hizo ni kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakuwa za kiwango na zenye kukidhi mahitaji ya wananchi.

Alieleza kuwa, unganishwaji umeme katika shule hiyo utasaidia kuboresha viwango vya ufaulu wa wanafunzi kwani kutakuwa na kambi ya kujisomea yenye uhakika wa usalama kutokana na uwepo wa mwanga muda wote.

Vilevile, alisema kupatikana kwa umeme katika zahanati ya Kata ya Makata, itasaidia kuboresha huduma za afya zinazotolewa kwenye zahanati hiyo ambapo huduma hizo zitapatikana kwa muda wote na hakutakuwa na kisingizo cha kutotoa huduma kwa sababu ya giza.

Pia, aliwataka wananchi wa vijiji hivyo, pamoja na kutumia umeme kwa matumizi ya nyumbani, wautumie pia katika kujiletea maendeleo kwa kujiajiri na kufanya shughuli mbalimbali za kujipatia kipato.

"Tumieni umeme kujiletea maendeleo. Kazi ya umeme ni pamoja na usalama majumbani, uboreshaji wa huduma za afya, kukuza uchumi kwa mtu mmoja mmoja, kwa jamii, familia na wilaya. Nataka Liwale iende mbali kiuchumi na nawaalika wawekezaji wakubwa na wadogo waje kuwekeza kwa sababu kuna umeme wa uhakika," alisema.

Naye Mbunge wa Liwale, Zuberi Kuchauka aliishukuru serikali kwa kufanya kazi kubwa ya usambazaji umeme nchini na kupeleka huduma hiyo wilayani humo.

Aliahidi kuwa wananchi wa jimbo lake watautumia umeme kwa usahihi ili kujiletea maendeleo.




*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu akizungumza na wananchi wa Kata ya Liwale Mjini, Wilaya ya Liwale, Mkoa wa Lindi, kabla ya kuwasha umeme katika shule ya msingi ya kata hiyo hivi karibuni. Kulia ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Sarah Chiwambwa.*



*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu akikata utepe kuashiria kuwashwa kwa umeme kwenye Shule ya Msingi Naluleo iliyopo katika Kata ya Liwale Mjini, Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi hivi karibuni.*



*Naibu waziri wa Nishati, Subira Mgalu akifurahi pamoja na kina mama wa kijiji cha Makata, mara baada ya kuwashwa kwa umeme kwenye zahanati ya kijiji hicho kilichopo Kata ya Makata, Wilaya ya Liwale, Mkoa wa Lindi hivi karibuni.*



*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (katikati), akisikiliza taarifa ya hali ya umeme wilayani Liwale, Mkoa wa Lindi. Anayewasilisha taarifa ni Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Liwale Festo Nhembo wakati akiwa kwenye ziara ya kazi ya ukaguzi wa kazi ya usambazaji umeme hivi karibuni.*



*Wananchi wa kijiji cha Makata wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (hayupo pichani), alipokuwa akihutubia kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini hapo akiwa katika ziara ya kazi kukagua usambazaji umeme kijijini humo hivi karibuni.*

# KATIBU MKUU NISHATI AHAMASISHA TAMISEMI ITUMIKE KUWAFIKIA WANANCHI



*Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (kushoto), akipokea nyaraka mbalimbali za Ofisi kutoka kwa mtangulizi wake, Dkt Hamisi Mwinyimvua katika hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika Februari 7, 2020 katika Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma.*



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kulia), akipokea nyaraka mbalimbali kutoka kwa Katibu Mkuu mstaafu, Dkt Hamisi Mwinyimvua katika hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika Februari 7, 2020 katika Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma.*

***Veronica Simba – Dodoma***

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Zena Said, ametoa hamasa kwa watumishi wa Wizara husika na Taasisi zake, kuwatumia viongozi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) katika kuwafikishia huduma wananchi.

Amesema kuwa kwa kuwatumia Wakuu wa Mikoa, Wilaya na viongozi wa Halmashauri, kutaleta matokeo chanya kwani wao hushughulika moja kwa moja na wananchi kuanzia ngazi ya chini kabisa, hivyo wanatambua namna bora zaidi ya kuwafikia.

Mhandisi Zena aliyasema hayo Februari 7, 2020 wakati akizungumza na Menejimenti ya Wizara pamoja na Wakuu wa Taasisi zilizo chini yake, muda mfupi baada ya kukabidhiwa rasmi Ofisi na mtangulizi wake, Dkt Hamisi Mwinyimvua.

"Tunahitaji kutumia muundo uliopo wa Serikali Kuu na zile za Mitaa ambazo watu wanalipwa lakini bado hawatumiki vizuri. Chochote tutakachofanya kama Wizara, tukitumia Serikali za Mitaa katika kufanya kampeni za uelimishaji, itatusaidia sana," alieleza.

Akifafanua zaidi, Katibu Mkuu aliwaeleza viongozi hao kuwa, siyo jambo la busara kufanya kazi kwa kujitenga kwani itakuwa ngumu lakini kwa kuwatumia watendaji husika itawasaidia kurahisisha kazi.

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu alisisitiza umuhimu na ulazima wa watumishi wote kuzingatia kanuni, sheria na taratibu mbalimbali zilizowekwa ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hivyo kila mmoja kwa nafasi yake kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Pombe Magufuli katika kuwahudumia wananchi ipasavyo.

Aidha, alihimiza utendaji kazi jumuishi yaani kama timu moja huku akitahadharisha kuwa, mmojawao akiharibu kazi kwa kutowajibika, atakuwa ameiangusha Wizara nzima.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya wafanyakazi wa wizara, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja, alimpongeza na kumshukuru Katibu Mkuu mstaafu Dkt Mwinyimvua kwa utendaji kazi mahiri na kuahidi ushirikiano kwa Katibu Mkuu mpya, Mhandisi Zena.

"Dkt Mwinyimvua, tunaamini Ofisi hii umeiacha katika mikono salama ya Mhandisi Zena. Mimi binafsi pamoja na watumishi wenzangu, tunaahidi kumpa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake."

Awali, akizungumza kabla ya kukabidhi Ofisi, Katibu Mkuu mstaafu Dkt Mwinyimvua aliahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa watendaji wote wa Wizara wakati wowote watakapomuhitaji.

Mhandisi Zena Said na Mhandisi Leonard Masanja, waliteuliwa na kuapishwa na Rais John Magufuli, Februari 3, mwaka huu katika nafasi ya Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu. Kabla ya uteuzi, Mhandisi Zena alikuwa ni Katibu Tawala Mkoa wa Tanga na Mhandisi Masanja alikuwa ni Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati.



*Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, akizungumza na Menejimenti ya Wizara pamoja na Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini yake, muda mfupi baada ya kukabidhiwa rasmi Ofisi na mtangulizi wake, Dkt Hamisi Mwinyimvua (hayupo pichani), katika hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika Februari 7, 2020 katika Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma.*



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, akizungumza katika hafla fupi ambapo yeye pamoja na Katibu Mkuu mpya wa Wizara, Mhandisi Zena Said walikabidhiwa rasmi Ofisi na Katibu Mkuu Mstaafu, Dkt Hamisi Mwinyimvua Februari 7, 2020 katika Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma.*



*Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na mtangulizi wake, Dkt Hamisi Mwinyimvua (kushoto) na Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Leonard Masanja (kulia), baada ya makabidhiano rasmi ya Ofisi yaliyofanyika Februari 7, 2020 katika Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma.*

# MATUKIO PICHANI



*Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (kushoto) na Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Leonard Masanja, wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kukabidhiwa rasmi Ofisi na Katibu Mkuu Mstaafu, Dkt Hamisi Mwinyimvua, katika hafla fupi iliyofanyika Februari 7, 2020 katika Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma.*




*Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (mbele-katikati), Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Leonard Masanja (mbele-kulia) na Katibu Mkuu mstaafu, Dkt Hamisi Mwinyimvua (mbele-kushoto), wakiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti ya Wizara pamoja na Wakuu wa Taasisi zilizo chini yake, mara baada ya makabidhiano rasmi ya Ofisi yaliyofanyika Februari 7, 2020 katika Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma.*



*Kutoka kulia ni Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja na Katibu Mkuu mstaafu, Dkt Hamisi Mwinyimvua, wakifurahia jambo muda mfupi kabla ya makabidhiano rasmi ya Ofisi yaliyofanyika Februari 7, 2020, Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma.*











*Matukio mbalimbali wakati wa mapokezi ya Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, alipowasili katika Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma, Februari 7, 2020.*

# MATUKIO PICHANI




*Matukio mbalimbali wakati wa mapokezi ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Leonard Masanja, alipowasili katika Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma, Februari 7, 2020. Mhandisi Masanja aliteuliwa katika nafasi hiyo na kuapishwa na Rais John Magufuli Februari 3, 2020 pamoja na Katibu Mkuu mpya Mhandisi Zena Said.*





*Matukio mbalimbali wakati wa mapokezi ya Katibu Mkuu mstaafu wa Wizara ya Nishati, Dkt Hamisi Mwinyimvua, alipowasili katika Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Dodoma, Februari 7, 2020 kwa ajili ya kukabidhi rasmi Ofisi kwa Katibu Mkuu mpya, Mhandisi Zena Said.*








*Menejimenti ya Wizara ya Nishati pamoja na Wakuu wa Taasisi zilizo chini yake, wakifuatilia hafla fupi ya makabidhiano ya Ofisi kutoka kwa Katibu Mkuu mstaafu, Dkt Hamisi Mwinyimvua (hayupo pichani) kwenda kwa Katibu Mkuu mpya, Mhandisi Zena Said na Naibu wake, Mhandisi Leonard Masanja (hawapo pichani), Februari 7, 2020 Mtumba Dodoma.*

# TANESCO WATAKIWA KUHAMIA KWENYE MAJENGO YAO

*Veronica Simba – Chato*

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani ametoa maagizo kwa uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kuhakikisha wanahamisha Ofisi zao zilizo katika majengo ya kupanga na kuhamia katika majengo yao yanayojengwa sehemu mbalimbali nchini.

Dkt Kalemani alitoa maagizo hayo Februari 25 mwaka huu baada ya kutembelea eneo zinapojengwa ofisi za TANESCO wilayani Chato, Mkoa wa Geita ambapo alisisitiza kuwa, mwisho wa kutekeleza agizo hilo ni Aprili 31, 2020.

Alisema lengo la kujenga Ofisi hizo ni kusogeza huduma kwa wateja ili waweze kuhudumiwa kwa wakati pamoja na kuwapunguzia kero ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa pili-kushoto), akitoa maelekezo kwa Wakandarasi wanaosimamia ujenzi wa Jengo la Ofisi za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wilaya ya Chato, alipotembelea kujionea maendeleo yake, Februari 25 mwaka huu.*

"Mheshimiwa Rais ametuelekeza tusogeze huduma kwa wananchi. Nasi kama Wizara, tumejipanga vizuri kupitia TANESCO kutekeleza maagizo hayo."

Akielezea zaidi kuhusu manufaa ya ujenzi husika hususan kwa wilaya ya Chato, Dkt Kalemani alisema kabla ya ujenzi, wananchi walikuwa wanalazimika kufuata huduma Geita na Biharamulo.

Alisema, jengo hilo litakapokamilika, litahudumia wananchi wa Chato na maeneo jirani hususani yanaopakana nayo, ambayo ni pamoja na Biharamulo, Ngara na Bukombe.

Kuhusu Mkandarasi anayejenga jengo hilo, Waziri alieleza kuwa ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), ambapo baada ya kufanya ziara hiyo alimwelekeza kufanya kazi usiku na mchana pamoja na kuongeza idadi ya vibarua ili akamilishe kazi husika ifikapo Aprili mwaka huu badala ya Juni kama ilivyo kwenye mkataba.

Akizungumzia uamuzi wa serikali kuitaka TANESCO kuondoka kwenye majengo ya kupanga, Waziri alisema utasaidia kuokoa fedha nyingi za shirika zilizokuwa zikitumika kulipia kodi lakini pia itawezesha shirika kumiliki mali zake ambazo zinaweza kutumika hata katika mikopo kwa ajili ya uendeshaji wake.

Ujenzi wa majengo mbalimbali ya Ofisi za TANESCO unaendelea nchini kote hususan katika maeneo ambayo shirika hilo lilikuwa limepanga katika majengo ya watu binafsi.

Imeelezwa kuwa idadi ya majengo hayo ya TANESCO yanayoendelea kujengwa inafikia 42 nchi nzima.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (aliyeinua mikono-kulia), akitoa maelekezo kwa wakandarasi wanaosimamia ujenzi wa Jengo la Ofisi za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), alipotembelea eneo hilo, Februari 25 mwaka huu.*



*Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa Jengo la Ofisi za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wilayani Chato, wakati Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) alipotembelea eneo hilo kujionea maendeleo yake Februari 25, mwaka huu.*

*Taswira ya jengo la Ofisi za Shirika la Umeme Tanzania, Wilaya ya Chato linalojengwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). Taswira hii ilichukuliwa Februari 25, 2020 wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani).*





*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa tatu-kulia), akijadiliana jambo na Msimamizi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), wilayani Chato, Mhandisi Gladys Jefta kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (wa tatu-kushoto). Waziri alizuru eneo hilo kujionea maendeleo ya ujenzi huo, Februari 25 mwaka huu.*



*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu akisalimiana na baadhi ya viongozi wa kijiji cha Kiromba, Kata ya Kiromba, Wilaya ya Mtwara Vijijini, Mkoa wa Mtwara, wakati akiwa kwenye ziara ya kazi kukagua maendeleo ya usambazaji umeme kijijini humo hivi karibuni.*



*Wananchi wa Kijiji cha Ushirika, Kata ya Mangochapanne wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza nao katika mkutuno wa hadhara uliofanyika kijijini humo hivi karibuni.*

# SERIKALI IMEJIPANGA KUONDOA KASORO ZILIZOJITOKEZA KWENYE MIRADI YA REA - MGALU

***Hafsa Omar - Mtwara***

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu amesema serikali kupitia Wizara ya Nishati na taasisi zake zinazohusiana na umeme imejipanga kikamilifu kuhakikisha inaziondoa kasoro ambazo zilijitokeza kwenye miradi ya Umeme Vijijini (REA) katika awamu zilizopita.

Aliyasema hayo Februari 26, 2020 wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kiromba, Kata ya Kiromba, Wilaya ya Mtwara vijijini, mkoani Mtwara, kabla ya kuwasha umeme kwenye kijiji hicho.

Alizitaja baadhi ya kasoro hizo kuwa ni pamoja na baadhi ya wakandarasi kupewa maeneo makubwa ya mikoa miwili hadi mitatu tofauti, yenye ukubwa tofauti, ambapo ilisababisha baadhi yao kutokufanya kazi kwa ufanisi.

Nyingine ni kurukwa kwa baadhi ya vijiji wakati wa kuunganisha umeme ambapo alisema katika awamu ijayo ya utekelezaji wa miradi hiyo ya umeme vijijini, haitakubalika kuona baadhi ya vijiji vikirukwa.

Aliongeza kuwa, serikali imedhamiria kurekebisha mapungufu mbalimbali yaliyojitokeza katika miradi iliyopita ili utekelezaji wake katika awamu zijazo uwe wenye tija zaidi.

"Katika mradi wa Peri-Urban, tuliweka Mkandarasi tofauti kwa kila wilaya ambapo kila mmoja amejielekeza kwenye wilaya yake. Hii imesaidia sana. Katika miradi ijayo, Serikali inadhamiria kupitia sheria za manunuzi, kwamba walau kila mkandarasi apewe kiasi anachokimudu kwa wakati ule kwa sababu hatuna muda mwingi na tunatakiwa 2021 tukamilishe kazi."

Pia, aliwatoa hofu wananchi wa Mkoa wa Mtwara kwa kuwaeleza kuwa maeneo yote ambayo bado umeme haujafika yataingizwa kwenye orodha ya kazi zinazoendelea na kuwahakikishia kuwa fedha zipo kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini na kupitia wadau mbalimbali wa maendeleo ambao wameridhishwa na jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali ili kuwaletea maendeleo Watanzania.

Vilevile, alisema serikali haitakubali tena kuona maeneo ambayo yapo barabarani lakini hayana umeme. Amesema kuwa maeneo yote ya aina hiyo yanatakiwa kupelekewa umeme kwa haraka zaidi.

Aidha, alisema pindi Mradi wa REA III, Awamu ya Kwanza, Mzunguko wa Pili utakapokamilika, Serikali itaanza kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji na kazi hiyo itakuwa ni rahisi kwa sababu umeme mkubwa utakuwa umefika kwenye kila Kata.

Naye Zahara Juma, mkazi wa kijiji hicho ambaye amejiajiri kwenye duka la madawa, aliiomba serikali iendelee kusambaza umeme vijijini ili kurahisisha utoaji wa huduma za kijamii kwa wananchi.

Katika ziara hiyo, Naibu Waziri pia aliwasha umeme katika Kijiji vya Mwenge, Kata ya Kiyanga, Kijiji cha Ushirika Kata ya Mangopachanne na Kijiji cha Kitere Kata ya Kitere, wilayani Mtwara Vijijini.



*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mwenge, Kata ya Kiyanga, Wilaya ya Mtwara vijijini, Mkoa wa Mtwara (hawapo pichani), wakati akiwa kwenye ziara ya kazi kukagua maendeleo ya usambazaji umeme kijijini humo hivi karibuni.*



*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (aliyeshika Mkasi) akikata utepe kuashiria kuwashwa kwa umeme katika kijiji cha Kiromba,kata ya Kiromba, Wilaya ya Mtwara vijijini Mkoa wa Pwani.*



*Mkazi wa Kijiji cha Mwenge, Kata ya Kiyanga, wilayani Mtwara Vijijini, Zahara Juma (aliyeshika kipaza sauti), akitoa neno la shukrani mara baada ya Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (wa pili-kushoto) kuwasha rasmi umeme katika kijiji hicho hivi karibuni.*

# DKT KALEMANI AAGIZA KITUO CHA KUPOZA UMEME NYAKANAZI KIKAMILIKE NOVEMBA



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akiangalia mchoro wa ramani ya kituo cha kupoza umeme kinachojengwa Nyakanazi, wilayani Biharamulo alipotembelea eneo hilo Februari 25, kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi husika.*



*Msimamizi wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme Nyakanazi, Mhandisi Elias Makunga (wa tatu-kulia), akifafanua jambo kwa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati) kuhusu maendeleo ya mradi huo. Waziri alitembelea eneo hilo kujionea maendeleo yake, Februari 25, 2020.*

**Veronica Simba – Biharamulo**

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amewaagiza wakandarasi wanaotekeleza mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme kilichopo Nyakanazi wilayani Biharamulo, kukamilisha kazi hiyo ifikapo Novemba mwaka huu badala ya Januari 2021, kama ilivyo kwenye mkataba.

Pia, ameagiza mradi mwingine unaotekelezwa sambamba na huo ukihusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi, ukamilike Januari 2021 badala ya Machi mwaka huo.

Alitoa maagizo hayo Februari 25 mwaka huu, alipotembelea eneo kinapojengwa kituo hicho cha kupoza umeme, ambacho ni sehemu ya mradi mkubwa wa kusafirisha na kusambaza umeme unaotekelezwa na serikali kutoka Kigoma – Nyakanazi – Geita – Bulyanhulu kwa gharama ya shilingi bilioni 93.27 za Tanzania.

Akifafanua sababu za kutoa maelekezo hayo, Dkt Kalemani alisema ni kutokana na umuhimu wa kukamilika kwa mradi huo mapema ambao unatarajiwa kutatua changamoto mbalimbali za upatikanaji umeme ambazo wamekuwa wakizipata wakazi wa maeneo husika.

Sambamba na hilo, pia Waziri alisema ni kutokana na imani aliyonayo kwa Mkandarasi husika (M/s Kalpataru Power Transmission Limited – India) kutokana na historia ya kazi alizotekeleza awali hapa nchini.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akitoa maelekezo kwa uongozi wa TANESCO na wakandarasi wanaotekeleza mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi, Februari 25 mwwaka huu, alizuru eneo hilo lililopo wilayani Biharamulo kujionea maendeleo yake.*

"Hii kampuni inayojenga mradi wa kusafirisha umeme, ndiyo ilijenga mradi wa Makambako – Songea na walikamilisha kazi mwezi mmoja kabla ya mkataba kuisha kama nilivyowaelekeza. Kutokana na uzoefu walionao, naamini hata kazi hii wana uwezo wa kuikamilisha kabla ya muda."

Akieleza zaidi kuhusu mradi husika, Waziri Kalemani alisema ni kati ya miradi mikubwa ya vielelezo katika masuala ya kuzalisha, kufua, kusafirisha pamoja na kusambaza umeme ambayo inatekelezwa na serikali.

Kuhusu utekelezaji wake, Waziri alieleza kuwa umegawanyika katika sehemu tatu, ya kwanza ikihusisha mikoa ya Iringa – Mbeya mpaka Tunduma (kilovoti 400), ambapo utekelezaji wake umeshaanza.

Alisema sehemu ya pili ni kutoka Sumbawanga kupitia Mpanda hadi Kigoma ambapo kwa upande wa Kigoma (Kidahwe) kutajengwa Kituo kikubwa cha kupoza umeme.

"Sehemu ya tatu ya mradi ndiyo hii kutoka Kigoma kuja hapa Nyakanazi umbali wa kilomita 280 na kutoka hapa mpaka Geita umbali wa kilomita 144, pamoja na kutoka Geita hadi Bulyanhulu, umbali wa kilomita 57."

Aidha, aliongeza kuwa, mradi huo pia utaungana na mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo wenye megawati 27 kwa kila nchi husika (Tanzania, Rwanda na Burundi). Alisema, itajengwa njia ya kusafirisha umeme kutoka Nyakanazi hadi Rusumo, umbali wa kilomita 96.

Vilevile, Waziri Kalemani alieleza kuwa, Mradi huo utasambazia umeme vijiji takribani 31 ambako unatekelezwa kutoka Nyakanazi kupitia Bwanga (Chato) na maeneo mbalimbali kwenda Katoro/Buseresere hadi Bulyahulu na kuongeza kuwa wananchi wataunganishwa kwa gharama ya umeme vijijini (REA), ambayo ni shilingi 27,000 tu.

Alitumia fursa hiyo kuwaalika wawekezaji mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kujitokeza kuwekeza katika maeneo yote unakotekelezwa mradi akiwahakikishia kuwa kutakuwa na umeme wa uhakika, unaotabirika na baadaye wenye gharama nafuu.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Wilaya ya Biharamulo Venance Martin, akimwakilisha Mkuu wa Wilaya, alipongeza mikakati ya kusambaza umeme inayotekelezwa na serikali huku akitolea mfano wa mradi huo ambao alisema mbali na kuwanufaisha wananchi, utawezesha kukuza uchumi wa viwanda katika ukanda husika.

Msimamizi wa Mradi huo (Geita-Nyakanazi), Mhandisi Elias Makunga, alisema maagizo ya Waziri yanatekelezeka na alimhakikishia kuwa atasimamia utekelezaji wake ipasavyo.

Katika ziara hiyo Waziri alifuatana na viongozi na wataalamu mbalimbali akiwemo Mwakilishi wa Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Dauson Kamaka, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mhandisi Raymond Seya, na Msimamizi wa Miradi ya REA Kanda ya Ziwa, Mhandisi Ernest Makale.

# MATUKIO PICHANI



*Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Raymond Seya (katikati), akijadiliana jambo na Meneja wa shirika hilo Kanda ya Ziwa, Mhandisi Maclean Mbonile (kushoto) na Meneja wa Wilaya ya Biharamulo, Ernest Milyango wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), eneo kunapojengwa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi, wilayani Biharamulo, Februari 25, 2020.*





*Kazi ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi wilayani Biharamulo ikiendelea. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani kujionea maendeleo ya mradi huo, Februari 25 mwaka huu.*



*Msimamizi wa miradi ya Umeme Vijijini (REA) Kanda ya Ziwa, Mhandisi Ernest Makale (kushoto) akiongozana na wakandarasi na wataalamu wengine kutoka TANESCO, wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), eneo kunapojengwa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi, wilayani Biharamulo, Februari 25, 2020.*

# WAZIRI KALEMANI ATOA RAI KWA KATIBU MKUU MPYA NISHATI



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati) akisisitiza jambo wakati wa kikao kilichojumuisha uongozi wa Wizara na wafanyakazi kwa lengo la kuwakaribisha rasmi viongozi wapya ambao ni Katibu Mkuu, Mhandisi Zena Said (kushoto kwa Waziri) na Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja (kushoto kwa Katibu Mkuu). Kulia kwa Waziri ni Naibu Waziri, Subira Mgalu. Kikao hicho kilifanyika Februari 7, 2020 Makao Makuu ya Wizara, Mtumba Dodoma.*

**Veronica Simba – Dodoma**

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amemtaka Katibu Mkuu mpya, Mhandisi Zena Said, kulipa kipaumbele suala la kukutana na watumishi wa Wizara pamoja na Taasisi zake, ili kusikiliza changamoto wanazokabiliana nazo na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema, kwa kufanya hivyo itasaidia kuwajengea watumishi hao utulivu wa kisaikolojia hivyo watatekeleza majukumu yao ya kuwahudumia watanzania kwa ufanisi zaidi.

Alikuwa akizungumza katika kikao maalum cha viongozi na watumishi wa Wizara, kilicholenga kumkaribisha rasmi Katibu Mkuu mpya pamoja na Naibu wake, Mhandisi Leonard Masanja, kilichofanyika Februari 7, 2020 Makao Makuu ya Wizara, Mtumba Dodoma.

"Simaanishi kwamba changamoto za watumishi zilikuwa hazishughulikiwi, la hasha, lakini kila mtu ana namna yake ya utekelezaji. Hayo ndiyo maelekezo yangu kwako," alisema Waziri.

Akifafanua, Dkt Kalemani alisema kuwa changamoto kwa watumishi ni jambo la kawaida mahala pa kazi lakini ni muhimu kuzitatua kwa wakati, kwani zinapoachwa kwa muda mrefu husababisha utendaji mbovu unaozorotesha utoaji huduma kwa wananchi na kurudisha nyuma maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Katika hatua nyingine, Waziri alimtaka Katibu Mkuu kutumia uzoefu wake katika masuala ya manunuzi ili aisaidie Wizara katika eneo hilo na kuiepusha na migogoro ya aina hiyo ambayo hutokea katika mashirika na taasisi mbalimbali za serikali.

"Tusaidie kusimamia na kutatua mapema ili isitokee migogoro ambayo itatupotezea muda wa kuwahudumia wananchi. Unapotumia muda mwingi kushughulikia migogoro unakosa muda wa kufanya mambo ya msingi kama kupeleka umeme kwa wananchi hivyo kurudisha nyuma jitihada za Serikali."

Vilevile, Waziri alimwelekeza Katibu Mkuu kusimamia miradi mbalimbali inayotekelezwa chini ya Wizara kwani inalenga kuwahudumia wananchi kwa kuhakikisha kunakuwepo na nishati ya uhakika na yenye gharama nafuu huku akisisitiza kwamba sekta ya nishati imebeba dhamana kubwa kwa wananchi maana inagusa maisha yao moja kwa moja.

Pamoja na maelekezo hayo kwa Katibu Mkuu mpya, Waziri alieleza wazi kuwa Wizara ina imani na matumaini makubwa kwake kutokana na historia yake ya utendaji kazi katika sehemu zote alikopita.

Sambamba na hilo, alimpongeza Naibu Katibu Mkuu Masanja na kumwelezea kuwa ni mfano wa kuigwa kutokana na utendaji kazi wake mahiri aliouonesha akiwa mtumishi wa Wizara husika kwa nafasi mbalimbali.

Alimtaka kushirikiana na Katibu Mkuu pamoja na viongozi wengine katika kuwaongoza watumishi kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu, pamoja na kuwapongeza Katibu Mkuu na Naibu wake, alitoa shukrani kwa Rais John Pombe Magufuli kwa uteuzi alioufanya ambao alisema umeipatia Wizara ya Nishati viongozi makini na wachapa kazi.

"Binafsi nafurahi zaidi kwani uteuzi umewezesha kuleta uwiano wa kijinsia (50/50) ambapo suala hili liko katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM)."

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Waziri na Naibu Waziri walimpongeza Katibu Mkuu aliyestaafu, Dkt Hamisi Mwinyimvua kwa utendaji kazi mzuri ambao umeiwezesha Wizara ya Nishati kufanya vizuri katika kutekeleza miradi mbalimbali.

Awali, akizungumza katika mkutano huo, Katibu Mkuu mpya, alishukuru kwa mapokezi mazuri lakini akaahidi kufanya kazi kwa bidii na pia akaomba ushirikiano kutoka kwa viongozi na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

"Naamini uzoefu nilioupata katika utumishi wa umma na sehemu nyingine mbalimbali nilizofanya kazi, utanisaidia kutekeleza majukumu yangu kama Katibu Mkuu pasipo shaka yoyote."

Alikiri kuwa Wizara ya Nishati inategemewa na wananchi kwa sababu inagusa maisha yao. Aliahidi kuendeleza pale mtangulizi wake alipoishia kwa kushughulikia malengo ya Wizara na Serikali kwa ujumla, ambayo ni pamoja na kupeleka umeme vijijini.

"Hadi sasa tumefanya vizuri lakini naamini tunaweza kufanya vizuri zaidi," alisema.

Katibu Mkuu mpya na Naibu Katibu Mkuu, waliteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Pombe Magufuli hivi karibuni na kuapishwa Februari 3, mwaka huu.



*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (kushoto) akitoa salamu za pongezi kwa viongozi wapya wa Wizara ambao ni Katibu Mkuu, Mhandisi Zena Said (wa pili kutoka kulia) na Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Leonard Masanja (kulia) katika kikao maalum kilichojumuisha viongozi wa Wizara na watumishi ambacho kilifanyika Februari 7, 2020 Makao Makuu ya Wizara, Mtumba Dodoma. Wa pili kutoka kushoto ni Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani.*



*Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (aliyesimama-kulia), akizungumza wakati wa kikao maalum cha viongozi na wafanyakazi wa Wizara kilicholenga kumkaribisha rasmi yeyé pamoja na Naibu wake, Mhandisi Leonard Masanja (kushoto kwa Katibu Mkuu). Katikati ni Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na kulia kwake ni Naibu Waziri Subira Mgalu. Kikao hicho kilifanyika Februari 7, 2020 Makao Makuu ya Wizara, Mtumba Dodoma.*













*Baadhi ya viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Nishati wakiwa katika kikao maalum cha kuwakaribisha viongozi wapya ambao ni Katibu Mkuu Mhandisi Zena Said na Naibu wake, Mhandisi Leonard Masanja. Kikao hicho kilifanyika Februari 7, 2020 Makao Makuu ya Wizara, Mtumba Dodoma.*

# NAIBU WAZIRI NISHATI AVIWASHIA UMEME VIJIJI SITA MKOANI MTWARA



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akisalimiana na viongozi mbalimbali wa Kijiji cha Kipimi, Kata ya Makota, Wilaya ya Newala, Mkoa wa Mtwara, akiwa kwenye ziara ya kazi kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini hivi karibuni.



Wananchi wa kijiji cha Kikuyu, Kata ya Mahumbika, Wilaya ya Newala, Mkoa wa Mtwara, wakifurahia ujio wa Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (hayupo pichani), aliyetembelea kijiji hicho hivi karibuni akiwa katika ziara ya kazi.

***Hafsa Omar - Mtwara***

Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu, Februari 25 mwaka huu aliwasha umeme katika vijiji sita vilivyopo katika Wilaya za Newala na Tandahimba, mkoani Mtwara.

Vijiji hivyo ni Kilidu, Mmovo, Kipimi, Kikuyu (Newala), Nakayaka na Tandika ambavyo vipo katika Wilaya ya Tandahimba.

Akizungumza na waandishi wa habari, mara baada ya kuwasha umeme kwenye vijiji hivyo, Naibu Waziri alipongeza jitihada za Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, kukutana mara kwa mara na wakandarasi wa miradi ya Umeme Vijijini (REA) na kufanya nao vikao ambapo alibainisha kuwa imesaidia Mkandarasi huyo kufanya kazi kwa haraka zaidi.

Aidha, alisema amepata matumaini kuona kazi za usambazaji umeme zinaenda vizuri ambapo wananchi wengi wameunganishiwa umeme na Mkandarasi husika kuvuka idadi ya wateja iliyokuwepo.

Alisema, kupatikana kwa wateja wengi katika miradi hiyo ni fursa kubwa kwa Wizara ya Nishati na taasisi zake zinazohusika na masuala ya umeme katika kuendeleza sekta hiyo.

"Miradi hii ikimalizika tutaikabidhi kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). Tunachotegemea sasa kutoka kwao ni kazi ya usambazaji maana tutakuwa tumewakabidhi mtaji wa wateja na miundombinu maana yake tumewakabidhi fedha."

Alieleza kuwa, Serikali imejipanga kutoa huduma ya umeme wa uhakika katika mikoa ya Mtwara na Lindi na kwamba kwa kuzingatia hilo imechukua hatua mbalimbali za kuboresha kituo cha kuzalisha umeme cha Mtwara kwa kukiongezea mashine mbili mpya ili kukiwezesha kutoa huduma kwa ufanisi.

"Wananchi wanataka umeme wa uhakika. Siyo unamunganishia leo, kesho umeme unanza kukatika na kuunguza vitu vyao vya thamani. Serikali tumejipanga na tutahakikisha tunatoa umeme wa uhakika," alisema Mgalu.

Katika hatua nyingine, aliwatoa hofu watumiaji wa gesi nchini kwa kueleza kuwa Serikali ipo katika hatua ya mazungumzo ya kuhakikisha bidhaa hiyo inayotumika majumbani inaagizwa kwa pamoja kama inavyofanyika kwenye mafuta.

"Tumepima mafanikio ya utaratibu huo na kujiridhisha kuwa umewezesha kushusha bei ya mafuta. Tutafanya hivyo pia katika uingizaji wa gesi."

Alifafanua kuwa, kwa utaratibu wa uagizwaji gesi pamoja itasaidia nishati hiyo kuingia kwa wingi tena kwa pamoja nchini, ambapo itasaidia kukua kwa soko lake na matumizi ya gesi yataoengezeka.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akiwapungia mikono kwa furaha wananchi wa Kijiji cha Mmovo, Kata ya Muungano, Wilaya ya Newala, Mkoa wa Mtwara, akiwa kwenye ziara ya kazi kukagua maendeleo ya usambazaji umeme vijijini hivi karibuni.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Nakayaka, Kata ya Chikongola, Wilaya ya Tandahimba, mkoani Mtwara (hawapo pichani) alipozuru kijiji hicho akiwa katika ziara ya kazi hivi karibuni.

# UMEME WAONGEZA UFAULU KWA WANAFUNZI LINDI

*Veronica Simba – Lindi*

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga amesema kuwashwa kwa umeme katika vijiji mbalimbali vya wilaya hiyo, kumeongeza ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne na cha pili katika shule za sekondari.

Aliyasema hayo Februari 12, 2020 mbele ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, kwenye hafla ya uwashaji umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Mpenda, Halmashauri ya Mtama, wilayani Lindi.

"Mheshimiwa Waziri, naomba nikuhakikishie kuwa ahadi aliyoitoa Mkuu wa Shule ya Sekondari Namangale, siku ulipokuwa unawasha umeme katika shule hiyo, imetimia. Shule hiyo na nyingine tisa (9) ambazo umeziwashia umeme hazina tena division 0," alisema.

Mkuu huyo wa Wilaya aliishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutekeleza ahadi zake ambazo alisema zimekuwa zikiboresha maisha ya wananchi katika nyanja mbalimbali ikiwemo kiuchumi.

Akieleza zaidi kuhusu manufaa ambayo wananchi wamekuwa wakiyapata kutokana na nishati ya umeme, alisema mbali na kuboresha elimu, uwepo wa umeme pia umeboresha huduma katika sekta mbalimbali zikiwemo afya na maji.

"Hapa Mpenda, baada ya wewe kusema unawasha umeme, watu wa maji nao wamejitokeza na kusema wanaleta maji, maana sasa wamekuwa na uhakika kuwa umeme upo."

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Kalemani alikiri kufurahishwa na taarifa ya Mkuu wa Wilaya kuwa umeme umeleta matokeo chanya katika elimu na sekta nyingine mbalimbali wilayani humo.

Alimwagiza Mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Umeme Vijijini Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza (REA III, Phase 1), kuhakikisha anaongeza idadi ya magenge ili kusambaza umeme katika vitongoji mbalimbali ambavyo havijafikiwa.

Aidha, Waziri alimtaka Mkandarasi huyo ambaye ni Kampuni ya State Grid Electrical & Technical Works Ltd, kuhakikisha anakamilisha kazi yote katika wigo aliopewa ifikapo mwishoni mwa mwezi Aprili mwaka huu na kuikabidhi kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), ambapo Mkandarasi husika aliahidi kutekeleza agizo hilo.

Katika ziara hiyo mkoani Lindi, Waziri Kalemani pia aliwasha umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Ng'au, Kata ya Mnacho wilayani Ruangwa pamoja na kukagua hali ya upatikanaji umeme na kuzungumza na wananchi wa Kijiji cha Nandagala wilayani Ruangwa.

Akiwa Ruangwa, Waziri alipokea salamu za shukrani kwa Rais John Magufuli kutoka kwa wananchi ambazo ziliwasilishwa na Mkuu wa Wilaya Hashim Mgandilwa, zikieleza kuridhishwa na utendaji kazi mahiri ambao umewapatia maendeleo hususan katika sekta ya umeme.

Kwa nyakati tofauti alitoa pongezi kwa wabunge wa maeneo hayo ambao ni Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (Ruangwa) na Nape Nnauye (Mtama) kwa kazi nzuri wanazofanya katika kuhakikisha wananchi wao wanapata umeme.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka TANESCO Lindi, maendeleo ya Mradi wa REA III – 1 kwa ujumla katika mkoa huo, hadi kufikia Februari 2020, ni asilimia 99 ambapo kazi mbalimbali zimetekelezwa.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akiwasha umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Mpenda, Halmashauri ya Mtama, mkoani Lindi, Februari 12, 2020.*




*Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga akitoa salamu za shukrani kwa Serikali mbele ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), kutokana na upelekaji umeme vijijini wakati wa hafla ya kuwasha umeme katika kijiji cha Mpenda wilayani humo, Februari 12, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akikata utepe kabla ya kuwasha rasmi umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Mpenda, Halmashauri ya Mtama, mkoani Lindi, Februari 12, 2020. Kulia kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga.*

# MATUKIO *PICHANI*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati) akifurahi pamoja na wananchi baada ya kuwasha umeme katika Zahanati ya kijiji cha Mpenda, Halmashauri ya Mtama, mkoani Lindi, Februari 12, 2020.*



*Sehemu ya wananchi na wauguzi wa Zahanati ya Kijiji cha Mpenda, Halmashauri ya Mtama, Mkoa wa Lindi, wakimsikiliza Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), wakati wa hafla ya kuwasha umeme katika Zahanati hiyo, Februari 12, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kushoto), akikabidhi kifaa cha Umeme Tayari (UMETA) kwa wananchi wakati wa hafla ya kuwasha umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Ng'au, Kata ya Mnacho, wilayani Ruangwa, Mkoa wa Lindi, Februari 12, 2020. Waziri alisisitiza vifaa hivyo vitumike kuunganisha umeme katika taasisi za umma.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa kijiji cha Ng'au, Kata ya Mnacho, wilayani Ruangwa, Mkoa wa Lindi, wakati wa hafla ya uwashaji umeme Februari 12, 2020.*

# MRADI WA UJENZI BOMBA LA MAFUTA MBIONI KUANZA



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akiwa na Waziri wa Nchi ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mussa Zungu, katika hafla ya kukabidhi Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa Mradi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), iliyofanyika katika ofisi za Makamu wa Rais jijini Dodoma hivi karibuni.*



*Kutoka kushoto ni Mratibu wa Mradi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Wizara ya Nishati, Salum Mnuna, Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi na Meneja wa Mradi huo, Martin Tiffen wakiwa katika hafla ya kukabidhi Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa EACOP, iliyofanyika hivi karibuni, Ofisi ya Makamu wa Rais iliyopo Mtumba jijini Dodoma.*

**Hafsa Omar - Dodoma**

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani amesema kuwa ujenzi wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima Uganda mpaka Tanga Tanzania (EACOP) unaendelea kutekelezwa kama ulivyopangwa na tayari nchi zote mbili zipo kwenye hatua za utekelezaji.

Aliyasema hayo, Februari 6, 2020 wakati wa hafla ya kukabidhi cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa Mradi huo iliyofanyika katika ofisi za Makamu wa Rais, jijini Dodoma.

Alieleza kuwa, tayari hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa na Serikali ya Tanzania ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kama ulivyopangwa. Alizitaja kuwa ni pamoja na kupata eneo ambalo litatumika kuweka matanki makubwa manne ya mafuta katika Kata ya Chongoleani, mkoani Tanga.

Hatua nyingine mbazo Serikali imezichukua ni upatikanaji wa korido ambayo ni njia ya kupitishia bomba yenye kilomita 1,414 kwa upande wa Tanzania na kwa ujumla wake zitakuwa 1,443 zikijumlishwa na kilomita 300 za upande wa nchi ya Uganda.

Aliongeza kuwa, hatua nyingine ni ukamilishaji wa kazi ya tathmini ya fidia kwa wale wote watakaopisha eneo la korido hilo ambalo litapita katika wilaya zaidi ya 24, kata 86 na vitongoji 278.

Aliendelea kueleza kuwa, kazi ambazo kwa sasa Serikali inazifanya ni pamoja na majadiliano baina ya nchi mbili husika kuhusu manufaa halisi ya kiuchumi na kijamii katika pande zote mbili, ambapo ajira zaidi ya 5,000 zitapatikana kutokana na mradi huo zikijumuisha ajira za kudumu na zisizo za kudumu.

Alisema kuwa, ujenzi wa mradi huo utaanza rasmi mara tu baada ya kukamilika kwa majadiliano na matayarisho husika na kwamba ujenzi wa mradi huo utachukua takribani miezi 36.

Vilevile, alisema jambo hilo la makabidhiano ya cheti cha tathmini lilikuwa likisubiriwa kwa muda mrefu ambapo sasa limefungua fursa ya kuanza kwenda katika hatua ya utekelezaji wa mradi huo mkubwa.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu alisema kuwa hafla hiyo ni ushahidi wa Serikali kuridhia Mradi husika ambapo itahakikisha masuala ya kiuchumi, kijamii, mazingira, afya na usalama, yanashughulikiwa wakati wote wa kipindi cha kupanga, kujenga na uendeshaji wa shughuli za bomba ili kupunguza athari kwa mazingira.

Pia, alisema mradi huo umezingatia maeneo muhimu ya kimazingira kama vile mbuga za wanyama, maeneo tengefu kama vile hifadhi za misitu na maeneo yenye idadi kubwa ya watu.

Aliongeza kuwa, vituo vitawekwa na kuendeshwa kwa umakini ili kupunguza athari yoyote ya kimazingira na kiikolojia wakati wa utekelezaji wa Mradi huo ambao unahitaji ushirikiano baina ya pande tatu ambazo ni Serikali za Tanzania na Uganda pamoja na wawekezaji.

Aidha, alisema kazi ya Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), haiishii kutoa Cheti tu, bali kuendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wake kulingana na masharti ya Cheti kilichotolewa.

"Timu yangu imejipanga na itaendelea kushirikiana na Wizara ya Nishati ambayo ni Msimamizi na Mratibu wa Sekta ya Mafuta na Gesi Tanzania pamoja na wawekezaji pindi watakapoanza kutekeleza Mradi huu kwenye hatua ya ujenzi na uendeshaji ili kuhakikisha kwamba mradi unatekelezwa kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira,"alisema.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Wizara ya Nishati na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira pamoja na Menejimenti ya Mradi wa EACOP.



*Waziri wa Nchi ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Zungu akizungumza katika hafla ya kukabidhi Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa Mradi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), iliyofanyika hivi karibuni katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Mtumba jijini Dodoma.*

# MATUKIO *PICHANI*



*Baadhi ya viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Nishati wakiwa katika kikao maalum cha kuwakaribisha viongozi wapya ambao ni Katibu Mkuu Mhandisi Zena Said na Naibu wake, Mhandisi Leonard Masanja. Kikao hicho kilifanyika Februari 7, 2020 Makao Makuu ya Wizara, Mtumba Dodoma.*




*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akikata utepe kwenye nyumba ya Mzee Juma Siki (aliyeshika utepe) kuashiria kuwashwa kwa umeme katika kijiji cha Kikuyu, Kata ya Mahumbika, Wilaya ya Newala, Mkoa wa Mtwara, akiwa katika ziara ya kazi hivi karibuni.*



*Wananchi wa Kijiji cha Tandika, Kata ya Dinduma, Wilaya ya Tandahimba, mkoani Mtwara, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (hayupo pichani), alipokuwa akizungumza nao akiwa katika ziara ya kazi hivi karibuni.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akizungumza katika hafla ya kukabidhi Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa Mradi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) iliyofanyika hivi karibuni, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mtumba jijini Dodoma.*




*Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Samuel Gwamaka akimkabidhi Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa Mradi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), Meneja wa Mradi huo Martin Tiffen.*



*Viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano pamoja na Menejimenti ya Mradi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya makabidhiano ya Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa Mradi huo, yaliyofanyika hivi karibuni, Ofisi ya Makamu wa Rais iliyopo Mtumba jijini Dodoma.*

# CCM CHATO YASEMA WAZIRI KALEMANI AMEITENDEA HAKI ILANI

***Veronica Simba – Chato***

Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Chato kimekiri kuridhishwa na utendaji kazi wa Waziri wa Nishati ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo hilo, Dkt Medard Kalemani.

Ameyasema hayo Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM, Wilaya ya Chato, Ramadhani Ndaki na kuongeza kuwa kwa utendaji kazi wake mahiri, Dkt Kalemani ameitendea haki Ilani ya Chama hicho ambacho ndicho kinaongoza nchi.

Kiongozi huyo wa Chama alikuwa akizungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya Waziri Kalemani kuwasha rasmi umeme katika kijiji cha Bukamila, Kata ya Kigongo, Februari 22, 2020.

"Utendaji kazi mzuri wa Dkt Kalemani umetupa matumaini sisi viongozi kuwa Ilani ya Chama inatekelezwa ipasavyo na kwakweli wakati ukifika, tutamtendea haki," amesema Ndaki.

Akifafanua zaidi kuhusu utendaji kazi wa Dkt Kalemani, Ndaki alieleza kuwa, akiwa ni Waziri mwenye dhamana ya nishati, pamoja na mambo mengine, amefanya bidii kubwa kuhakikisha wananchi hasa walioko vijijini nchi nzima wanafikiwa na umeme.

Kwa upande wa Chato, Ndaki alieleza kuwa Dkt Kalemani amefanya makubwa katika sekta ya nishati ambapo mpaka sasa Kata zote 23 za Jimbo hilo zimekwishafikiwa na umeme.

Awali, akizungumza katika mkutano wa hadhara na wananchi wa kijiji hicho cha Bukamila, Dkt Kalemani alibainisha kuwa hadi sasa jumla ya vijiji takribani 9,000 vimekwishaunganishiwa umeme nchini kati ya 12,268 vilivyopo, sawa na asilimia 74.

Aliwahakikishia watanzania kuwa hadi kufikia Oktoba mwaka huu, jumla ya vijiji 10,446 vitakuwa vimeunganishwa na umeme na kwamba ifikapo Juni 2021, vijiji vyote vya Tanzania Bara vitakuwa vimefikiwa na nishati hiyo.

Alimpongeza na kumshukuru Rais John Magufuli kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya umeme nchini na akaahidi kuwa yeye na viongozi wenzake waandamizi wa Wizara, wataendelea kusimamia vyema matumizi yake kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.



*Katibu wa Siasa na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi, Wilaya ya Chato, Ramadhani Ndaki, akizungumza wakati wa hafla ya kuwasha umeme katika kijiji cha Bukamila, Chato. Mgeni Rasmi katika hafla hiyo iliyofanyika Februari 22, 2020 alikuwa ni Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani).*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akifurahia mara baada ya kuwasha umeme katika kijiji cha Bukamila, wilayani Chato, Februari 22, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akizungumza wakati wa hafla ya kuwasha umeme katika kijiji cha Bukamila, wilayani Chato, Februari 22, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kushoto), akiwatambulisha viongozi waandamizi kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), mbele ya wananchi wakati wa hafla ya kuwasha umeme katika kijiji cha Bukamila, wilayani Chato, Februari 22, 2020.*

# KIJIJI CHA MKANGE CHAANZA KUSAMBAZIWA UMEME

***Hafsa Omar - Pwani***

Wananchi wa mtaa wa Mkange uliopo katika Kata ya Mkange, wilayani Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, wameishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuzindua rasmi kazi ya usambazaji umeme wa Mradi wa Peri-Urban kwenye maeneo ambayo siyo miji wala vijiji katika kata hiyo.

Tukio hilo lilitokea, Februari 20, 2020 katika kata hiyo, wakati Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu alipokuwa kwenye ziara ya ukaguzi wa kazi ya usambazaji umeme vijijini na kuzindua rasmi kazi za usambazaji umeme kwenye kata hiyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wakazi wa eneo hilo waliishukuru serikali kwa kuona umuhimu wa kuwaletea umeme kwenye kata yao na kuongeza kuwa utawasaidia  kwa matumizi mbalimbali hasa katika huduma za jamii.



*Wananchi wa kata ya Mkange, wilayani Bagamoyo wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (hayupo pichani) wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye kata hiyo, hivi karibuni.*

Akizungumza katika mkutano wa hadhara kwenye kata hiyo, Naibu Waziri alisema kata hiyo ni moja kati ya kata ambazo huchangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Taifa, kwani ndiyo kata inayopatikana hifadhi ya Taifa ya Saadan.

Aidha, alisema kuanza rasmi kwa usambazwaji wa umeme ambao serikali imeugharamia kwa pesa nyingi, itakuwa fursa kwa wanakijiji hao kujikwamua kiuchumi. Aliwataka wananchi wa kata hiyo kuutunza mradi huo na wajitokeze kwa wingi kulipia shilingi 27,000 ili waweze kunganishiwa huduma hiyo.

"Nawaomba ndugu zangu tuombe mradi uende kwa wepesi. Ninyi mkikubali uende kwa wepesi utakwenda kwa wepesi. Ndiyo kwanza tunaianza safari sasa ya kuwasha taa ya kwanza katika kata hii kubwa ya Mkange."

Vilevile, aliwataka watendaji wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kutafuta wakandarasi wenye uwezo wa kufanya kazi kwenye maeneo yenye changamoto bila ya malalamiko husussan katika miradi itakayoanza hivi karibuni.

"Mmeona tumepita katikati ya mbuga. Mtakapokwenda kwenye taratibu za manunuzi msituletee wakandarasi wababaishaji. Tunataka wakandarasi wenye uwezo wa kuhimili maeneo kama hayo. Hatutaki mkandarasi ambaye atasema mvua inanyesha gari haipitiki,"alisisitiza.



*Mafundi wakiwa wanaendelea na kazi ya uwekaji nguzo za umeme, kata ya Mkange, Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (hayupo pichani), hivi karibuni.*



*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu akizungumza na wananchi wa kata ya Mkange, wilayani Bagamoyo, akiwa katika ziara ya kazi ya ukaguzi wa usambazaji umeme hivi karibuni.*



*Mafundi wakiwa tayari wameshachimbia nguzo za umeme katika eneo la kata ya Mkange, wilayani Bagamoyo tayari kwa kusambaza umeme. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nishati hivi karibuni.*



*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu na wananchi wa Kata ya Mkange, wilayani Bagamoyo, wakiwa wameshika nguzo ya umeme kuashiria kufika kwa nishati ya umeme katika eneo hilo hivi karibuni.*

# DODOMA ITAKUWA NA UMEME MWINGI KUPITA MIKOA YOTE NCHINI – WAZIRI KALEMANI



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kushoto), akitoa maelekezo kwa mkandarasi (Kampuni ya KCE) anayetekeleza mradi wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme Zuzu, Dodoma, alipofanya ziara kukagua maendeleo ya mradi huo, Februari 19, 2020.*

**Veronica Simba – Dodoma**

Serikali kupitia Wizara ya Nishati, inakamilisha mradi mkubwa wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme kilichopo Zuzu Dodoma, ambacho baada ya kukamilika kitakuwa na uwezo wa megawati zaidi ya 600, hivyo kuongoza Tanzania nzima kwa wingi wa umeme.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, Februari 19, 2020 alipofanya ziara katika kituo hicho kujionea maendeleo ya utekelezaji wa mradi husika.

Akizungumza na waandishi wa habari, Waziri alibainisha kuwa, kwa kiasi hicho cha umeme (megawati 640), Dodoma italipita hata jiji la Dar es Salaam ambalo linaongoza kwa sasa kwa kuwa na megawati takribani 587.

"Napenda niishukuru sana Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Rais kwa kutupatia Dola za Marekani milioni 52 kwa ajili ya kutekeleza mradi huu," amesema.

Akifafanua zaidi kuhusu manufaa ya mradi huo, Dkt Kalemani alisema mbali na kutosheleza mahitaji ya kawaida ya wananchi, kiasi hicho cha umeme pia kitawezesha uwekezaji wa viwanda vya aina mbalimbali hivyo kukuza uchumi.

Alieleza zaidi kuwa, dhamira ya serikali kutekeleza mradi huo ni kutokana na ongezeko la mahitaji ya umeme mkoani humu ambayo yamepanda kutoka wastani wa megawati 15 hadi kufikia megawati 40 kwa siku.

Alisema, ongezeko hilo la mahitaji linaweza kusababisha uhaba wa nishati ya umeme Dodoma endapo hazitachukuliwa hatua za makusudi na haraka katika kulitafutia ufumbuzi na kuongeza kuwa, ndiyo maana serikali imeagiza mradi huo ukamilike na kukabidhiwa ifikapo mwishoni mwa mwezi huu wa Februari, 2020.

"Kasi ya kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi Dodoma ni kubwa. Tukizembea, hali inaweza kuwa mbaya, jambo ambalo serikali haiwezi kuruhusu litokee.

Kufuatia umuhimu wa kukamilika kwa mradi huo mapema, Waziri alimtaka mkandarasi anayetekeleza mradi huo, kampuni ya KCE kutoka India, kufanya kazi usiku na mchana ili akamilishe kazi kwa wakati huku akisisitiza kuwa kamwe hataongezewa muda.

Katika hatua nyingine, Waziri aliuagiza uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kupitia kwa Msimamizi wa Mradi husika, Mhandisi Peter Kigadye, kushughulikia malalamiko ya wananchi wanaoishi jirani na Kituo hicho ambayo ni pamoja na kuunganishiwa huduma ya umeme pamoja na kuboresha miundombinu ya barabara.

Hii ni mara ya tatu kwa Waziri Kalemani kufanya ziara katika kituo hicho ili kujionea maendeleo ya mradi husika tangu ulipoanzwa kutekelezwa Machi, 2018.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akitoa maelekezo kwa mkandarasi (Kampuni ya KCE) anayetekeleza mradi wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme Zuzu, Dodoma, alipofanya ziara kukagua maendeleo ya mradi huo, Februari 19, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia), akitoa maelekezo kwa mkandarasi (Kampuni ya KCE) anayetekeleza mradi wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme Zuzu, Dodoma, alipofanya ziara kukagua maendeleo ya mradi huo, Februari 19, 2020.*

# WALIMU IPARAMASA WAISHUKURU SERIKALI KUWAPELEKEA UMEME



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akiwaasa wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi Tumaini, iliyopo Kata ya Iparamasa wilayani Chato, kutumia umeme kuboresha taaluma baada ya kuwasha rasmi nishati hiyo shuleni hapo Februari 24, 2020 akiwa katika ziara ya kazi.*



*Baadhi ya Walimu wa Shule ya Msingi Tumaini, iliyopo Kata ya Iparamasa wilayani Chato, wakifuatilia hafla ya uwashaji rasmi umeme shuleni hapo, Februari 24, 2020 ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani).*

**Veronica Simba – Chato**

Walimu wa Shule ya Msingi Tumaini iliyopo kijiji cha Imalabupina, Kata ya Iparamasa, wilayani Chato, Mkoa wa Geita, wameishukuru Serikali kwa kuunganisha umeme shuleni hapo wakisema nishati hiyo italeta mapinduzi makubwa ya taaluma.

Wametoa shukrani hizo Februari 24, 2020 baada ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani kuwasha rasmi umeme katika Shule hiyo.

Akieleza namna shule hiyo itakavyonufaika, Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule hiyo, Goodluck Mamele amesema uwepo wa umeme utarahisisha zoezi la uchapaji wa karatasi za mitihani na majaribio mbalimbali ambayo hufanyika mara kwa mara shuleni hapo.

Alisema, awali walikuwa wakilazimika kupeleka mitihani kwenye 'stationeries' kwa ajili ya kuchapisha huku wakiingia gharama kulipia huduma hiyo.

"Sasa naamini taaluma itapanda maana badala ya kuchangisha fedha za kuchapishia mitihani, tutaifanya kazi hiyo hapahapa shuleni."

Aidha, alisema uwepo wa umeme shuleni utawasaidia baadhi ya walimu ambao hawana elimu ya kutumia Kompyuta, kujifunza utaalamu huo katika muda wao wa mapumziko baada ya saa za kazi.

Kwa upande wake, Mwalimu Moses Manyilizu, amesema uwepo wa umeme utawezesha sasa kufundisha somo la TEHAMA kwa wanafunzi kwani awali mazingira yalikuwa siyo rafiki.

Kwahiyo, sasa hivi kwakuwa tuna umeme, najua kupitia Mfuko wa Shule, tutajitahidi kupata kompyuta kwa ajili ya kuwafundisha watoto somo la TEHAMA."

Naye Mwalimu Habi Nyanda ameeleza kuwa umeme utawawezesha wanafunzi wanaopenda kujisomea kwa muda wa ziada kufanya hivyo hata nyakati za usiku shuleni hapo hivyo kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu kwao.

Akizungumza baada ya kuwasha umeme, Waziri Kalemani amewaasa wanafunzi na walimu wa shule hiyo, kuitumia nishati hiyo kama chachu kwao katika kuboresha taaluma shuleni hapo.

Katika ziara hiyo, Waziri pia aliwasha umeme kwenye taasisi mbalimbali za umma na makazi ya wananchi katika vijiji vya Butobela na Mwendakulima vilivyopo Kata ya Butengolumasa.



*Sehemu ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Tumaini, iliyopo Kata ya Iparamasa wilayani Chato, wakifuatilia hafla ya uwashaji rasmi umeme shuleni hapo, Februari 24, 2020 ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani).*



*Mashine ndogo ya kusaga nafaka katika kijiji cha Butobela, Kata ya Butengolumasa, wilayani Chato ikiwa imeunganishwa umeme. Taswira hii ilichukuliwa Februari 24, 2020 wakati Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) alipokuwa akiwasha rasmi umeme eneo hilo.*

# MATUKIO *PICHANI*







*Taswira mbalimbali zikionesha hatua iliyofikiwa katika kutekeleza mradi wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme Zuzu, Dodoma. Taswira hizi zilinaswa Februari 19, 2020 wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani).*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake, wakikagua maendeleo ya mradi wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme Zuzu, Dodoma Februari 19, 2020.*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia), akizungumza na wananchi wanaoishi jirani na kituo cha kupoza umeme Zuzu Dodoma, alipokuwa katika ziara kukagua maendeleo ya mradi wa upanuzi wa kituo hicho, Februari 19, 2020.*



*Baadhi ya viongozi waandamizi na wataalamu kutoka Wizarani, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), wakifuatilia hafla ya uwashaji rasmi umeme katika Shule ya Msingi Tumaini iliyopo Kata ya Iparamasa, wilayani Chato, Februari 24, 2020 ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani).*



*Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Imalabupina, Kata ya Iparamasa, wilayani Chato. Kulwa Mapembe akimkaribisha Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa pili-kushoto), aliyefika kuwasha rasmi umeme katika Shule ya Msingi Tumaini iliyopo kijijini hapo, Februari 24, 2020 akiwa katika ziara ya kazi.*

# VIJIJI VYENYE UMEME CHATO VYAFIKA 114 KATI YA 115



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akiwasha rasmi umeme katika kijiji cha Rwantaba, wilayani Chato, Mkoa wa Geita, Februari 21, 2020 akiwa katika ziara ya kazi.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye miwani-katikati), akicheza ngoma ya Mlekule na akina mama wa kijiji cha Nyarutefye wilayani Chato, Mkoa wa Geita, wakati wa hafla ya kuwasha rasmi umeme, Februari 21, 2020.

**Veronica Simba – Chato**

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amewasha umeme katika vijiji vya Rwantaba na Nyarutefye vilivyopo Chato, mkoani Geita na kufanya idadi ya vijiji vilivyofikiwa na nishati hiyo wilayani humo kufikia 114 kati ya 115 vilivyopo.

Akizungumza na wananchi wa kijiji cha Nyarutefye, Februari 21, 2020, muda mfupi kabla ya kuwasha umeme, Waziri Kalemani alieleza kuwa ifikapo mwisho wa mwezi huu, vijiji vyote wilayani humu, vitakuwa na umeme.

Hata hivyo Waziri alibainisha kuwa, Chato haitakuwa Wilaya ya kwanza kuwashiwa umeme katika vijiji vyake vyote kwani tayari kuna jumla ya wilaya 34 nchini ambazo hadi sasa vijiji vyake vyote vimekwishafikiwa na huduma ya umeme.

Alieleza kuwa, serikali kupitia wizara yake inaendelea na zoezi la kuunganisha umeme vijijini nchini kote ambapo hadi kufikia mwezi Oktoba mwaka huu, jumla ya vijiji 10,446 vitakuwa vimeunganishwa kati ya 12,268 vilivyopo nchi nzima.

"Tutabaki na vijiji 1,822 ambavyo kufikia Juni 2021 vitakuwa vimeunganishwa na hivyo kufanya vijiji vyote nchini kuwa vimefikiwa na umeme."

Katika hatua nyingine, Waziri Kalemani aliwaasa wananchi ambao umeme umefika katika maeneo yao, kuchangamkia fursa hiyo kwa kulipia na kutandaza mfumo wa nyaya katika nyumba zao ili waunganishiwe.

Aidha, alisisitiza kuwa, umeme utumike kwa matumizi yenye tija zaidi hususan kiuchumi badala ya kuutumia kuwasha taa peke yake.

Akijibu hoja za baadhi ya wananchi ambao wamedai kutounganishiwa umeme pamoja na kwamba wameshalipia huduma hiyo, Dkt Kalemani aliuagiza uongozi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kuhakikisha wanawaunganishia umeme wote wenye changamoto ya aina hiyo katika kipindi kisichozidi siku 14.

Vilevile, aliwataka watendaji hao wa TANESCO nchi nzima, kuharakisha zoezi la ukarabati wa miundombinu ya umeme iliyoharibika kufuatia mvua kubwa zilizokuwa zikinyesha ili kuwaondolea wananchi adha ya ukosefu wa umeme.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Chato Charles kabeho, ambaye aliambatana na Waziri katika ziara hiyo, alipongeza utendaji kazi wa Serikali ya Awamu ya Tano kwani ahadi zake zinatekelezwa na wananchi wanashuhudia.

Katika ziara hiyo, Waziri pia aliambatana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Raymond Seya, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga pamoja na maafisa wengine waandamizi kutoka wizarani na katika taasisi hizo.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa pili-kulia), akitoa maelekezo kwa viongozi mbalimbali wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha wanaunganisha umeme katika baadhi ya maeneo ya kijiji cha Nyarututu wilayani Chato, Mkoa wa Geita ambao wakazi wake wamejenga nyumba nzuri lakini wanakosa nishati hiyo. Waziri alikuwa katika ziara ya kazi, Februari 21, 2020.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akikata utepe kabla ya kuwasha rasmi umeme katika kijiji cha Nyarutefye wilayani Chato, Mkoa wa Geita, Februari 21, 2020. Kushoto kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho na anayemfuatia ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Amos Maganga.

# WATAALAMU WA NISHATI SADC WAAZIMIA MAMBO TISA

*Zuena Msuya - Dar es Salaam*

Mwenyekiti wa Mkutano wa Watalaamu na Makamishna wanaohusika na masuala ya nishati kutoka Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), ambaye pia ni Kamishna wa Petroli na Gesi (Tanzania), Adam Zuberi amesema mkutano huo umepitisha kwa pamoja mapendekezo tisa yanayohusu masuala ya nishati katika nchi hizo.

Mkutano huo wa siku nne ulifanyika jijini Dar es Salaam kuanzia Februari 25 na kuhitimishwa Februari 28, 2020

Alisema mapendekezo hayo waliyokubaliana yatakabidhiwa kwa Makatibu Wakuu husika na baadaye kuwasilishwa katika mkutano wa Mawaziri wa masuala ya nishati kwa nchi za SADC unaotarajiwa kufanyika mwezi Mei mwaka huu ili kuyatolea maamuzi.

Wakati akifunga mkutano huo, Zuberi alitaja baadhi ya mapendekezo yaliyopitishwa kuwa ni pamoja na kuanzisha Mpango Kabambe wa Matumizi bora ya gesi asilia katika nchi za SADC.

"Tayari kuna mshauri mwelekezi ameshaanza kazi hiyo, lakini pili tumeamua kila nchi iendelee kuhamasisha nchi nyingine ili kusaini uanzishwaji wa Kituo cha Umahiri cha Kuendeleza Nishati Jadidifu na Matumizi bora ya Nishati kwa Nchi za SADC (SACREE) ili utekelezaji wake uanze," alisema Zuberi.

Mapendekezo mengine ni kuhamasisha utekelezaji wa miradi ya nishati kati ya nchi na nchi pamoja na uanzishwaji wa sera ya ushirikishaji wa wanawake katika shughuli za kiuchumi, pendekezo ambalo limeshaanza baada ya kupatikana mshauri mwelekezi.

Vilevile, alisema kuwa suala la uhamasishaji na utekelezaji wa pamoja wa matumizi bora ya Nishati Jadidifu pia lilijadiliwa kwa kina katika mkutano huo ambapo kila nchi wanachama walieleza umuhimu wake katika kulinda mazingira na kuhakikisha nchi zenye uhaba zinatumia vyanzo hivyo kwa nishati bora.

"Kwa hiyo maeneo hayo yamejadiliwa kwa kina, mjadala ulikwenda vizuri na kamati ikakubaliana kuwasilisha mapendekezo hayo katika Baraza la Mawaziri lijalo," alisema Zuberi.

Vilevile, mkutano huo ulijadili mchakato wa uanzishaji wa Kituo cha Umahiri cha Kuendeleza Nishati Jadidifu na Matumizi bora ya Nishati kwa Nchi za SADC (SACREE) pamoja na mapitio ya Itifaki ya Nishati ya 1996.

Pia, ulijadili utekelezaji wa Mpango Kabambe wa utekelezaji wa Matumizi ya Gesi asilia katika nchi za SADC pamoja na mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Sekta ya Nishati chini ya Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Miundombinu katika Mtangamano (RIDMP), utakaofikia tamati mwaka 2027.

Ikumbukwe kwamba Mkutano wa 39 wa Jumuiya hiyo ulifanyika Agosti 17 na 18, 2019, jijini Dar es Salaam na kukabidhi majukumu ya uongozi wa jumuiya hiyo kwa Rais wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli baada ya Rais wa Namibia, Hage Geingob kumaliza muda wake.

Hivyo katika mkutano wa 40 wa jumuia hiyo utakaofanyika nchini Msumbiji, Tanzania itakabidhi kijiti cha majukumu ya uongozi wa jumuiya hiyo kwa Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi baada ya Rais wa Tanzania, Dkt. John Pombe kumaliza muda wake.




*Mwenyekiti wa Mkutano wa Kamati ya Watalaam na Makamishna wa masuala ya nishati kutoka Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), ambaye pia ni Kamishna wa Petroli na Gesi (Tanzania), Adam Zuberi (kulia) akizungumza na wajumbe wa mkutano huo (hawapo pichani) wakati akifunga mkutano huo uliofanyika jijijini Dar es Salaam kwa siku nne, Februari 25-28, 2020.*



*Wataalam kutoka Wizara ya Nishati (Tanzania), Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Mbadala, Edward Ishengoma (kushoto), Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga (kulia) na Mhandisi Joyce Kisamo, wakifuatilia mada wakati wa ufungaji wa mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati wa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) uliofanyika Jijijni Dar es Salaam Februari 25 - 28, 2020.*



*Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Maandalizi ya Mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati wa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) uliofanyika Jijijni Dar es Salaam Februari 25 - 28, 2020 wakiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa kamati hiyo ambaye pia ni Kamishna Msaidizi wa Maendeleo ya Umeme, Mhandisi Styden Rwebangila (katikati) baada ya kumalizika kwa mkutano huo.*



*Mwenyekiti wa Mkutano wa Kamati ya Watalaam na Makamishna wa masuala ya nishati kutoka Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), ambaye pia ni Kamishna wa Petroli na Gesi (Tanzania), Adam Zuberi, akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufunga mkutano wa Wataalamu wa Masuala ya Nishati wa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) uliofanyika Jijijni Dar es Salaam, Februari 25 - 28, 2020.*

# UUNGANISHAJI UMEME VIJIJINI WILAYANI MBOGWE WAFIKIA ASILIMIA 85



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akiwasha umeme katika Kituo cha kuuza mafuta kilichopo kijiji cha Bugomba, wilayani Mbogwe, Mkoa wa Geita, alipokuwa katika ziara ya kazi Februari 27, mwaka huu.*

***Veronica Simba – Mbogwe***

Zoezi la kuunganisha umeme vijijini katika Wilaya ya Mbogwe, mkoani Geita, limefikia asilimia 85.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, alipokuwa katika ziara ya kazi wilayani humo, Februari 27 mwaka huu, ambapo aliwasha umeme katika vijiji vya Nyikonga na Bugomba.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na wananchi wa vijiji hivyo, Dkt Kalemani alisema kuwa idadi ya vijiji ambavyo havijafikiwa umeme katika wilaya hiyo ni 16 tu kati ya 85 vilivyopo na kwamba hadi sasa ni Kata moja pekee ndiyo haijafikiwa na umeme kati ya 17.

"Kazi kubwa sana imefanyika hivyo hatuna budi kuipongeza Serikali. Aidha, kazi inaendelea na ninawahakikishia kuwa hadi kufikia Juni mwakani, vijiji vyote vya Mbogwe vitakuwa vimeunganishiwa umeme.

Waziri alitoa shukrani kwa Rais John Magufuli kwa kutoa jumla ya shilingi bilioni 31 ili zitumike kuunganisha umeme katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Geita hivyo hakutakuwa na kisingizio chochote cha kushindwa kufikisha umeme Geita nzima ikiwemo Mbogwe.

Katika hatua nyingine, Dkt Kalemani alitoa hamasa kwa wananchi hususan wanaomiliki viwanda vidogo vidogo na biashara mbalimbali, ambao umeme umekwishafika katika maeneo yao, kulipia huduma hiyo ili waunganishiwe.

Akieleza zaidi, alisema wananchi hawapaswi kusita kulipia huduma hiyo kwa maelezo kuwa wanasubiri nguzo kwani hilo siyo jukumu lao.

"Haijalishi makazi au biashara yako iko umbali gani kutoka kwenye nguzo. Wewe kalipie kisha sisi tutaweka utaratibu wa kukufikia," alisisitiza Waziri.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Martha Mkupasi aliwaasa wananchi kutunza miundombinu ya umeme ili nishati hiyo iendelee kuwanufaisha kwa matumizi mbalimbali.

Alisema, uharibifu wa miundombinu husika siyo tu kwamba utawakosesha huduma hiyo wananchi wenyewe bali pia utarudisha nyuma jitihada za serikali katika kuwapelekea wananchi wake maendeleo kupitia nishati hiyo kutokana na hasara itakayopatikana.

"Umeme utatusaidia kupunguza gharama nyingi tulizokuwa tukitumia kununua mafuta ya taa, dizeli na matumizi mengine mbalimbali."

Mbunge wa Mbogwe, Augustine Masele ni kati ya viongozi walioshiriki ziara hiyo ya Waziri Kalemani, ambapo alimpongeza Rais Magufuli kwa kuwezesha kazi ya usambazaji umeme kwa wananchi wa vijijini kufanyika kwa kasi.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akikata utepe kabla ya kuwasha rasmi umeme katika Kituo cha kuuza mafuta kilichopo kijiji cha Bugomba, wilayani Mbogwe, Mkoa wa Geita, alipokuwa katika ziara ya kazi Februari 27, mwaka huu.*



*Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Martha Mkupasi (mwenye kipaza sauti), akihamasisha wananchi kutunza miundombinu ya umeme, muda mfupi kabla ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati) kuwasha rasmi umeme katika kijiji cha Bugomba wilayani humo, Februari 27, 2020.*



*Mbunge wa Mbogwe, Augustine Masele (kulia), akitoa shukrani kwa serikali kutokana na utekelezaji wa kasi wa miradi ya umeme vijijini jimboni kwake, muda mfupi kabla Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kushoto) kuwasha rasmi umeme katika kijiji cha Nyikonga, wilayani Mbogwe, Februari 27 mwaka huu.*

## Maafisa kutoka Wizara ya Nishati (Tanzania), wakiwa katika Mkutano wa Wataalam wa Masuala ya Nishati wa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SADC) uliofanyika jijini Dar es salaam, Februari 25 hadi 28 mwaka huu.













# **MATUKIO** *PICHANI*





*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akizungumza na baadhi ya vijana wa kijiji cha Buziku wilayani Chato, Mkoa wa Geita, akiwa katika ziara ya kazi, Februari 21, 2020.*



*Kutoka kushoto ni Katibu wa Waziri wa Nishati, Mhandisi Robert Dulle, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi Raymond Seya na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Amos Maganga wakijadiliana jambo wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), kijijini Buziku, wilayani Chato, Februari 21, 2020.*



*Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho akizungumza na wananchi wakati wa hafla ya kuwasha rasmi umeme kijijini Nyarutefye, wilayani Chato, Februari 21, 2020. Tukio hilo lilifanywa na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (Mwenye miwani - Meza Kuu).*



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Rwantaba, wilayani Chato, Mkoa wa Geita, wakati wa hafla ya kuwasha rasmi umeme kijijini hapo, Februari 21, 2020.*